



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Unapojibu tafadhali taja:

05/01/2024

Kumb NA. LD/NGHL/181/49  
Kamishna wa Ardhi Msaidizi,  
Mkoa wa Geita,  
S.L.P 848,  
GEITA.

**YAH: MAOMBI YA KAMPUNI YA KIGENI SOHRAB MINING COMPANY LIMITED  
KUMILIKISHWA ARDHI KWA AJILI YA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA  
YA MADINI.**

Tafadhali rejea somo hapo juu.

2. Halmashauri yetu imepata mwekezaji kutoka Nchini India kwa lengo la kuwekeza katika sekta ya madini ndani ya Wilaya yetu. Mwekezaji huyu ni Kampuni ya kigeni inayojulikana kwa jina la **SOHRAB MINING COMPANY LIMITED** ya Nchini India.

3. Kampuni hii imepata ridhaa ya kufanya kazi zake Tanzania kupitia wakala wa usajili wa makampuni Tanzania BRELA (**Certificate Of Incorporation of a Company No: 170735021**). Kampuni hii pia inatambuliwa na Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) na kupatiwa namba ya mlipa kodi (**Taxpayer Identification Number (TIN) 170-735-021**).

3. Eneo ambalo kampuni hii inategemea kumilikishwa na kufanya uwekezaji katika shughuli za madini limepangwa kwa ajili ya matumizi husika na lina ukubwa wa mita za mraba 46,586. Eneo liko katika Kijiji cha Isonda Kata ya Nyugwa.

Viambatisho.

1. Cheti cha usajili kuruhusu Kampuni kufanya kazi Tanzania.
2. Cheti cha usajili wa mlipa kodi kutoka TRA.
3. Mchoro unaoonyesha eneo na ukubwa wake.

Nawasilishwa kwako kwa hatua zaidi za kisheria.

Husna Toni  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
NYANG'HWALE.

MKURUGENZI MTENDAJI  
S.L.P 352  
NYANG'HWALE

**ENEO PENDEKEZWA KWAAJILI YA UWEKEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHENJUAJI WA DHAHABU  
LILILOKO KIJIKI CHA ISONDA KATA YA NYUGWA WILAYA YA NYANG'HWALE**

